/ISSN 0856 - 034X

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

***Supplement No. 47*** ***29th November, 2024***

***SUBSIDIARY LEGISLATION***

*To The Gazette of the United Republic of Tanzania No.44 Vol. 105 Dated 29th November, 2024*
Printed by The Government Printer, Dodoma by Order of Government

TANGAZO LA SERIKALI NA. 958 la tarehe 29/11/2024

SHERIA YA MISITU,

(SURA YA 323)

# NOTISI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 29)*

NOTISI YA KUSUDIO LA KUBADILI HADHI YA ENEO LA MSITU WA HIFADHI WA TAIFA RAU KUWA MSITU WA HIFADHI WA MAZINGIRA ASILIA RAU YA MWAKA 2024

KWA KUWA, eneo la Msitu wa Hifadhi Rau lilitangazwa chini ya Tangazo la Serikali Na. 341 la mwaka 1961 kuwa eneo la Msitu wa Hifadhi Rau;

NA KWA KUWA Waziri, kwa mamlaka aliyopewa chini ya kifungu cha 29 cha Sheria ya Misitu, Sura ya 323 anaona kwamba ni kwa maslahi ya umma kubadili hadhi eneo la Msitu wa Hifadhi wa Taifa Rau kuwa Msitu wa Hifadhi wa Mazingira Asilia Rau; na

NA KWA KUWA, Waziri kwa kuzingatia Sheria ya Misitu ambayo, pamoja na masharti mengine, inamtaka Waziri anapokusudia kubadili hadhi Msitu wa Hifadhi wa Taifa kuwa Msitu wa Hifadhi wa Mazingira Asilia kutoa notisi ya kusudio kwa umma kabla ya kutekeleza mamlaka hayo;

HIVYO BASI, Waziri anatamka kama ifuatavyo:

Jina

1. Notisi hii itajulikana kama Notisi ya Kusudio la Kubadili hadhi Msitu wa Hifadhi wa Taifa Rau kuwa Msitu wa Hifadhi wa Mazingira Asilia Rau ya Mwaka 2024.

Eneo

2. Eneo la hifadhi lililo ndani ya mipaka iliyoainishwa

linalopendekezwa kutangazwa

katika Jedwali linapendekezwa kubadilishwa hadhi kuwa Msitu wa Hifadhi wa Mazingira Asilia Rau.

Madhumuni ya tangazo

3. Madhumuni ya kubadili hadhi ya Msitu wa Hifadhi wa Taifa Rau ni-

(a) kulinda eneo ambalo linatambulika kwa thamani yake ya juu ya baioanuwai, lenye upekee wa mimea na wanyama, ikijumuisha aina za mimea na wanyama walio hatarini, baadhi yao wako katika hatari ya kutoweka; na

(b) kulinda eneo la msitu na matumizi endelevu ya rasilimali za misitu.

Uhalali wa Notisi

4.-(1) Notisi hii itakuwa halali kwa muda wa siku tisini kuanzia tarehe ya kuchapishwa katika Gazeti la Serikali.

(2) ) Ndani ya kipindi hicho cha siku tisini, mtu au kundi la watu au mwakilishi wao anaweza, kwa maandishi kuwasilisha pingamizi, maoni au madai ya haki yoyote inayotokana na sheria za kimila kuhusiana na ardhi au mazao ya msitu au haki yoyote iliyoainishwa kwenye sheria nyingine katika eneo ambalo linapendekezwa kutangazwa kuwa Msitu wa Hifadhi wa Mazingira Asilia Rau.

Uwasilishaji wa pingamizi

5. Pingamizi, maoni au madai yoyote dhidi ya kusudio la kubadili hadhi Msitu wa hifadhi wa Taifa Rau kuwa Msitu wa Hifadhi wa Mazingira Asilia Rau, yawasilishwe ndani ya siku tisini kuanzia tarehe ya kuchapishwa katika Gazeti la Serikali kwa Notisi hii kwa anuani ifuatayo:

Katibu Mkuu,<br>
Wizara ya Maliasili na Utalii,<br>
S.L.P. 1351,<br>
DODOMA.

JEDW ALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

WILAYA YA MOSHI
MSITU WA HIFADHI WA MAZINGIRA ASILIA RAU

Makadirio ya eneo: Hekta 584.44 au Kilometa za Mraba 58.44 Unakopatikana na Mipaka:

Eneo lote la hifadhi awali chini ya Eneo la Msitu wa Hifadhi wa Rau unaopatikana Wilaya ya Moshi katika Mkoa wa Kilimanjaro kama lilivyochorwa katika Ramani ya Idara ya Upimaji Na. Jb 2842 (Skeli 1:10,000) iliyohifadhiwa na Mkurugenzi wa Upimaji na Ramani na lenye mipaka ifuatayo:

*Tangazo la Serikali Na. 958 (Linaendelea)*



*Tangazo la Serikali Na. 958 (Linaendelea)*



Dodoma,
11 Novemba, 2024

PINDI HAZARA CHANA,
*Waziri wa Maliasili na Utalii*